



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA BUKOBA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.KGR/BMC/S.35/49/97

02/12/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (TANGAZO LINARUDIWA)

Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba anapenda kuwatangazia wataanzania wote wenye sifa kutuma maombi ya nafasi za kazi kama ifuatavyo:

1. MHUDUMU WA JIKONI DARAJA LA II - NAFASI 2

A: SIFA ZA MWOMBAJI:

- i) Aliyefaulu Elimu ya Kidato cha Nne (IV)
- ii) Awe na Cheti cha Mafunzo ya U hudumu wa Jikoni kutoka katika Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

B: MAJUKUMU YA MHUDUMU WA JIKONI DARAJA LA II

- i) Kusafisha vyombo vya kupikia
- ii) Kusafisha vyombo vya kulia chakula
- iii) Kusafisha sehemu ya kulia chakula
- iv) Kuwatarishia Wapishi/Waandazi vifaa vya kazi
- v) Kusafisha maeneo ya kupikia

C: MSHAHARA


Cheo cha Mhudumu wa Jikoni Daraja la II kina mshahara wa **TGOS A** kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA

- i) Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania
- ii) Waombaji wote wawe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45

- iii) Waombaji wote wawe hawajawahi kupatikana na kosa la jinai, kugushi vyeti au kufungwa jela.
- iv) Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (Referees) watatu wa kuaminka pamoja na namba zao za simu.
- v) Waombaji wote waambatishe nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha 1 (passport size) ya hivi karibuni iliyoandikwa jina la mwombaji nyuma.
- vi) Waombaji wote waambatishe nakala ya kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA
- vii) Testimonials "Transcripts", "Provisional Results", "Statement of results", na "Result Slips" hazitakubaliwa.
- viii) Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganifu na NECTA na NACTE
- ix) Mwisho wa kuleta maombi ni tarehe **08/12/2022 saa 9:30** mchana.
- x) Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa:-

**MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA,
S.L.P. 284,
BUKOBA.**



Hamid A. Njovu
**MKURUGENZI WA MANISPAA
BUKOBA**

**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
BUKOBA**

**Nakala: Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira,
www.ajira.go.tz**

**“ Tovuti ya Halmashauri ya Manispaa Bukoba,
www.bukobamc.go.tz**

“ Mbao za Matangazo